# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO

### Makete DVTC

### 2024

Simu: +255787326298

Nukushi: (022)2863408

P.O. BOX 138
MAKETE

maketedvtc@veta.go.tz

www.veta.go.tz

Kumb. Na; 12/12/2023

Ndugu

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA Makete DVTC Mwaka 2024

MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika

   Fani ya

   Katika ngazi Level One

   mwaka wa I Boarding
2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili - mitatu (2-3)
3. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 15/01/2024
4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa
6. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua
7. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo
8. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni
9. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyoambatanishwa na barua hii
10. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa. Fedha ikishalipwa hairudishwi. Kama fedha za tahadhali (caution Money) hazikutumika zitarudishwa
11. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo

ELISHA NKUBA
MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO
CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
S.L.P. 138
MAKETE

## MASHARTI YA NYONGEZA YA KUJIUNGA NA CHUO

Unatakiwa kununua au kuleta vifaa vfuatavyo kwa matumizi yako Chuoni amabavyo vitakaguliwa na waalimu.

( i) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi ya " Tetron".

(ii) Jozi mbili (2) ya vaiatu vyeusi vyua ngozi vyenye kisigino kifupi.

(iii) Vifaa vya somo la Hesabu (Mathematical set) na Daftari 8 kubwa (Counter Book).

(iv) Picha Mbili (Passport Size).

(V) Uje na Karatasi za kutolea kopi (Photocopy paper ream) moja ya A4.

(vi) Unatakiwa uje na "Safety Boot" kwa ajili ya Mafunzo ya karakana.Kwa fani ya (MB,MVM na CJ) hii ni lazima.

(vii) Nunua godoro kwa mwanafunzi wa bweni (2.5 "ft × 3' ×6' ft),Blanket,shuka mbili za rangi ya bluu,ndoo,sahani,kikombe cha chai,kijiko,Mto,viatu vya michezo na Nguo za michezo (Truck suti).

(Viii) Wakati wa kusajiliwa unatakiwa ufike na stakabaadhi ya malipo ya michango mingine (Bank pay inslip) picha tatu kipimo cha pasipoti,vivuli halisi vya vyeti na fomu ya uthibitisho wa afya toka kwa daktari wa Hospitali ya Serikali/inayotambuliwa na Serikali.

(ix) Unatakiwa kufuata Sheria na taratibu zote za Chuo kama zilivyoamabatanishwa kwenye barua hii.

(X) Nafasi yako kama mwanachuo itapotea endapo utashindwa kuripoti Chuoni wiki Mbili (2) zaidi baada ya tarehe ya kufungua Chuo.

(xi) Fika na barua hii siku ya kuripoti

(xii) Fedha zote kwenye jedwali hapo chini zitalipwa kupitia Namba ya Malipo ya Serikali (Control Number) utakayopewa Chuoni siku ya kwanza ufikapo Chuoni.

(xiii) Uje na Sweta moja la rangi ya kijani jeshi.

(Xiv) Kwa wanachuo wa Bweni uje na "Water Squeezer",Soft Bloom na Hard Bloom.

(Xv)Uje na Jembe kubwa na Mpini wake pamoja na Slesha au Reki.

(Xii)Uje na Cheti cha kuzaliwa kwa mwanafunzi mwenye umri chini ya Miaka 18 au **Namba ya NIDA** kwa mwanachuo mwenye umri zaidi ya miaka 18.

## JEDWALI LA MCHANGANUO WA MALIPO

| S/N | MAHITAJI | MWANAFUNZI WA KUTWA | | MWANAFUNZI WA BWENI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | MUHULA WA I | MUHULA WA II | MUHULA WA I | MUHULA WA II |
| 1. | Gharama za Nembo | 5,000/= | | 5,000/= | |
| 2. | Tahadhari (Caution Money) | 20,000/= | | 20,000/= | |
| 3. | Kitambulisho | 5,000/= | | 5,000/= | |
| 4. | Ada kwa Mwaka | 30,000/= | 30,000/= | 60,000/= | 60,000/= |
| 5. | Matibabu (Bima ya Afya) | 50,400/= | | 50,400/= | |
| 6. | Sare za Shule (Suruali Mbili) | 50,000/= | | 50,000/= | |
| 7. | OverCoat/Overal | 30,000/= | | 30,000/= | |
| 8. | Michezo | 10,000/= | | 10,000/= | |
| 9. | T-shirt | 17,000/= | | 17,000/= | |
| | **JUMLA KUU** | **217,400/=** | **30,000/=** | **247,400/=** | **60,000** |

**NB;**Malipo ya Bima ni lazima kwa Wanafunzi wote.

## MALIPO YA ADA NA MICHANGO MINGINE:

1. Malipo yote ya Ada yatalipwa kwa kutumia mfumo wa Malipo ya Serikali kwa kutumia **'CONTROL NUMBER'**. Hivyo kila mwanachuo atakayeripoti Chuoni atapaswa kwenda idara ya Uhasibu kwa ajili ya kupewa 'Control Number' itakayomwezesha kulipia Ada na Michango mingine. (Ikumbukwe kuwa kwa Mwanachuo wa kutwa Ada yake kwa mwaka ni Tsh.60,000/= kwa muhula ikiwa ni Tsh.30,000/=.Na kwa mwanachuo wa Bweni Ada yake kwa mwaka ni Tsh.120,000/=,kwa muhula ikiwa ni Tsh.60,000/=).
2. Pia ikumbukwe kuwa kwa mwanachuo wa Bweni gharama za michango mingine ni **Tsh.197, 000/=** (bila kujumuisha gharama za bima ya Afya). Na kwa wanachuo wa kutwa Gharama za michango mingine bila kujumuisha Gharama za bima itakuwa ni **Tsh.167, 000/=.**
3. Aidha pia wazazi/walezi mnakumbushwa kuwa ikiwa kuna uhitaji wa kulipa Ada kulingana na sehemu uliyopo basi anaweza kufanya mawasiliano ya moja kwa moja na idara ya Uhasibu ili kupatiwa **'Control number'** kupitia Namba za Simu zifuatazo - **0768274558 / 0714803729**. Pia wazazi/walezi mnahimizwa kutunza stakabadhi za malipo ya bank (Pay inslip) na kuziwasilisha Chuoni siku ya kuripoti.

## SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WA KUTWA NA BWENI

ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA AWALI YA UFUNDI KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO:-

1. **MAHUDHURIO**

   (a) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1.30 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1.30 wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni. **Adhabu kali itatolewa kwa wachelewaji.**

   (b) Mwanafunzi hatakiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na mwalimu (Mkuu wa sehemu/idara).

   (c) Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari/taarifa zifike chuoni, bila ya kufanya hivyo ni kosa.

   (d) Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi atanyimwa cheti cha kuhitimu.

2. **MAVAZI**

   (a) Sare ya chuo ni suruali ya Bluu na shati Jeupe mikono mifupi. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Wakati wote shati liwe limechomekewa.

   (b) Ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

   (c) Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni.

3. **USAFI WA MWILI**

   (a) Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili, mkufu na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo.
   Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali chuoni.

   (b) Nywele kwa wavulana

   (i) Zikatwe ziwe fupi sana, KIPARA hairuhusiwi kabisa.

   (ii) Ndevu haziruhusiwi.

(c) Nywele kwa wasichana; Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma.

(d) Kucha zisifugwe kabisa wala kupakwa rangi.

4. **WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE**

(a) Vitendo vyovyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au ya mwanafunzi mwenzake, hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

(b) Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakinunue kifaa chenyewe au ulete badala ya ulichokipoteza.

(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo/bwenini.

(d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

(e) Mwanafunzi yeyote atakayepotelewa/kupoteza mali yake yoyote binafsi mfano simu,mavazi,vyombo,vifaa vya darasani n.k ,basi chuo hakitahusika kwa namna yoyote ile na upotevu wa mali husika (ikumbukwe kuwa utunzaji wa mali za mwanachuo ni jukumu la mmiliki mwenyewe na sio jukumu la chuo).

5. **UGOMVI**

Ugomvi, kupigana na kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

6. **ULEVI**

Iwapo itabainika mwanafunzi amelewa, au kuonekana katika sehemu za kileo/mazingira ya chuo, anavuta bangi au madawa ya kulevya basi hatua kali za kisheria zitachukuliwa mara moja dhidi yake.

7 **MAPENZI**

(a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanafunzi hairuhusiwi kabisa.

(b) Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi wafanyakazi wa chuo bila kibali au ruhusa.

8. **MIGOMO**

Migomo ni mafuruku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

9. **LUGHA**

Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni kiingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kiingereza.Pia katika mazingira ya chuo lugha rasmi za mawasiliano ni kiingereza na Kiswahili pekee.

10. Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa Chuo mara moja.

11. Ni Marufuku kuonekana/kutumia simu wakati wa vipindi vya darasani.

**ONGEZEKO LA SHERIA KWA MWANACHUO WA BWENI**

12. Ruhusa ya kutoka Chuoni; Ni Jumamosi saa 7:30mchana hadi saa 12:00 jioni. Jumapili na siku za sikukuu ni saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni; majina yaandikwe kwenye kitabu cha kutoka na kuingia kilichopo lango kuu/ getini. Mhusika aweke muda wa kutoka na kusaini arudipo.

13. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuwa

na kitambulisho cha Chuo na atajiandikisha lango kuu na sare ya chuo. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kuwa na kitambulisho atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bweni au kufukuzwa chuoni.

14. Mwanafunzi atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya chuo bila kibali atasimamishwa masomo.

15. Haitaruhusiwa kupika chakula bwenini , na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali.

16. (a) Ni marufuku wanachuo wa kiume na wakike kutembeleana mabwenini.

(b) Hairuhusiwi KABISA kwa mwanachuo kuingia katika eneo wanamoishi wafanyakazi wa chuo bila ruhusa au kibali:

17. Hairuhusiwi kupeleka chakula bweninì. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu itatolewa.

18. Taa za madarasani na mabwenini zizimwe saa 4:00 za usiku.

19. Hakuna ruhusa kumkaribisha au kumlaza mgeni, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni au ndugu siku ya masomo ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu/matron/patron kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo.

- Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila Jumamosi kuanzia saa 7:00 mchana hadi saa 12:00 jioni na jumapili au siku za sikukuu kuanzia saa12:00 asubuhi mpaka 12:00 jioni **(ila ni marufuku kwa mgeni kuingia bwenini kwa namna yoyote ile).**

20. Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.

21. Hairuhusiwi kulala nje ya chuo. Iwapo ikitokea ruhusa itatolewa na ofisi ya Mkuu wa Chuo.

22. Ni marufuku kwa mwanachuo wa bweni kutumia vifaa vya umeme anapokuwa bwenini.mfano; **pasi,'heater','rice cooker','blender',jiko la umeme** au vifaa vingine vinavyofanana na hivyo.

23. Ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga kelele ambazo hazina sababu za msingi kwa wanafunzi wenzake anapokuwa bwenini (kelele,fujo n.k haviruhusiwi).

24. Ni marufuku kukutwa na vifaa vinavyoweza kutumika kama silaa katika mazingira ya bweni.

**MKUU WA CHUO**

**CHUO CHA UFUNDI STADI VETA MAKETE**

**VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY**
**MAKETE DISTRICT VOCATIONAL TRAINING CENTER**

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Admission to MAKETE DVTSC is conditional upon receipt of satisfactory medical report. The practitioner to whom this form is presented is requested to examine the candidate to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an.......................................... (Trade)

The Medical Officer

.....................................

.....................................

.....................................

.....................................

Please examine .................................................... (Candidates name)

(i) Eyesight.....................................................

(ii) Hearing.....................................................

(iii) Height.....................................................

(iv) Allergies.....................................................

(v) Weight.....................................................

(vi) Asthma.....................................................

(vii) Epilepsy.....................................................

(viii) Other serious diseases...................................

MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

TITLE.................................................SIGNATURE.......................

Official Stamp..................................... Date.................................

BANDIKA PICHA
YA PASIPOTI
HAPA

TAARIFA YA MWANACHUO

## SEHEMU (A)

*Ijazwe na mwanafunzi (tumia herufi kubwa)*

1. Jina la ukoo ..........................................................................................
2. Majina Mengine ....................................................................................
3. Mahali ulipozaliwa (Wilaya) .......................................... (Kijiji/Mji) ..................................
4. Kiwango cha elimu ................................................................................
5. Tarehe na mwaka wa kuzaliwa ..............................................................
6. Hali ya ndoa (nimeoa/olewa) Sijaoa/olewa ..........................................
7. Anuani ya kudumu ................................................................................
8. Jina la mzazi/mlezi ................................................................................
9. Namba ya simu .....................................................................................

UTHIBITISHO

Mimi .................................................................. nathibitisha kwamba, nimekubali nafasi na kwamba taarifa nilizozijaza ni za kweli/sahihi kwa kadiri ya ufahamu wangu. Sahihi: ........................................... Tarehe: ................................

## SEHEMU (B)

*Ijazwe na Mzazi/Mlezi/Mdamini*

Mimi ......................................................................... S.L.P .............. Namba ya simu ya mkononi .......................................

Ninathibitisha kuwa ni mdhamini mtajwa hapo juu na nitalipia gharama zote za Mafunzo (ada) n.k pamoja na nauli wakati wote wa kwenda Chuoni na kurudi nyumbani kwa likizo na baada ya Mafunzo ya awali.

Tarehe: ............................................... Sahihi: .......................................

Uhusiano.........................................................

VET DECL FORM -1F

## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

a) MWANACHUO

Mimi ..........................................................................................ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

Sahihi...........................................................Tarehe.......................................

b) MDHAMINI

Mimi.........................................................ambaye.........................................wa mtajwa hapo juu nathibitisha kuwa nitamdhamini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ni ada na gharama nyingine kama ilivyoelekezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo na nauli ya kwenda chuoni na kurudi nyumbani wakati wote wa likizo na baada ya mafunzo.

Sahihi...........................................................Tarehe..................................